





Mimi naitwa Sesi, nina umri wa miaka sita. Ninasoma darasa la kwanza katika shule ya msingi ya Manyinga.



Siku yangu ya kwanza
shuleni, ilikuwa nzuri sana.
Niliamka asubuhi sana, baba
alinipeleka shuleni. Njiani
niliwaona wanafunzi
wenzangu wakiwa na wazazi
wao.



Mara nikasikia kengele inalia
ngo! Ngo! Ngo! Wanafunzi
wengine walikimbia mbio.



Nilipowaangalia, io! Nilijiona niko mdogo peke yangu. Wengine wote ni wakubwa, warefu.

Kila mmoja alisimama katika nafasi yake kwa mstari. Nami nilikimbia mbio kuwafuata, nilisimama nao.



Dada mmoja mkubwa alikuja, akanishika mkono. Alinipeleka kwa wanafunzi wenzangu.



Niliposimama nikasikia sauti nyuma yangu “mama huyu amejikojolea.” Wote tukageuka nyuma, Nilimwona mwanafunzi mdogo. Ameshikilia kaptura yake.



Miguu yake yote imelowa.
Machozi yanamtoka. Kaka
mkubwa akaja, akamchukua.
Sijui alienda nae wapi.



Mwalimu alituonesha darasa
letu lilikuwa kubwa na safi.
Aliingia mwanafunzi
mwingine amechelewa.
Ameshika viatu mkononi.



Mwalimu alimuuliza, kwa nini amevua viatu. Alisema mama yake humwambia kuvua viatu, anapoingia ndani ya nyumba, wote tukacheka.



Kengele ikalia tena ngo!
Ngo! Ngo! Tukakimbia,
tukasimama kwenye mstari.
Lakin hatukuwaona
mwanafunzi wengine ila sisi
tu. Mwalimu akaja
akatuambia, sasa ni
mapumziko hatusimami
kwenye mistari.



Baada ya muda kengele iligonga tena. Kila mwanafunzi alikimbia mbiombio. Sikujua niende wapi, kwani nimesahau darasa langu.



Nikaliona darasa mbele
yangu niliingia. Wenzangu
wawili wakanifuata.



Tulipotaka kukaa tu, walikuja akina dada watatu. Mmoja alituuliza, tunatoka wapi? Mmoja wetu akaanza kulia. Dada mkubwa alimuuliza kwa nini analia. Akasema anataka kwenda kwa mama yake. Wanafunzi wengine wakacheka.




Mwanafunzi mkubwa
alitupeleka darasani kwetu.
Mwalimu aliingia tena
darasani. Alituambia
kengele itakapogongwa
tusitoke
nje. Tuwangoje wazazi wetu
watufruate.



Kengele ikalia tena ngo, ngo,
ngo! Wengine walismama
walitaka kwenda nje. Wote
tulifurahi, tulipowaona
wazazi wetu wakitungojea.



Baba na mama waliniambia, nisikilize vizuri maelekezo ya walimu. Baada ya kumaliza chakula cha usiku. Baba na mama waliniuliza habari za shuleni. Niliwasimulia kuwa tulipotea darasa, walicheka sana.



Usiku niliona hauishi.
Nilitamani kuona siku yangu
ya pili shuleni.

